HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/2018 PAMOJA NA MPANGO WA MUDA WA KATI 2017/2018 – 2019/2020

IMETAYARISHWA NA:

HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO,
S.L.P. 55068,
DAR ES SALAAM
SIMU: 0222926341
FAX: 0222926342

APRILI, 2017

UBUNGO MUNICIPAL COUNCIL

ALL CORRESPONDENCES TO BE ADDRESSED TO THE MUNICIPAL DIRECTOR

Tel: 0222926341

Fax: 0222926342

MUNICIPAL DIRECTOR
UBUNGO MUNICIPAL COUNCIL
P. O. BOX 55068
DAR ES SALAAM

Date 13rd Aprili, 2017

THE LOCAL GOVERNMENT FINANCES ACT, 1982 (ACT NO. 9 OF 1982) APPROVAL CERTIFICATE
Issued Under Section 43

At its Full Council meeting held on 29th February, 2017, we the Councillors of UBUNGO MUNICIPAL COUNCIL under the powers conferred upon us by Section 43 of the Local Government Finances Act No. 9 of 1982, do hereby **approve the Estimates of Recurrent Revenue, Expenditure and Development Budget of UBUNGO MUNICIPAL COUNCIL** for the financial year 2017/2018.

SIGNATURE

NAME: BONIFACE JACOB

DATE: ……

SIGNATURE: 

NAME: JOHN LIPESI KAYOMBO

DATE: ……

UBUNGO MUNICIPAL MAYOR **UBUNGO MUNICIPAL DIRECTOR**

YALIYOMO

1 MUHTASARI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2017/2018 NA MPANGO WA MUDA WA KATI 2017/2018 – 2019/2020 1
1.1 UTANGULIZI 1
 TAMKO LA MHESHIMIWA MSTAHIKI MEYA 2
 MAELEZO YA MKURUGENZI WA MANISPAA 4
2 SURA YA KWANZA: UCHAMBUZI WA KIMAZINGIRA 12
2.1 TASWIRA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO 12
2.2 MAHALI ILIPO NA MUONEKANO WA KIJIOGRAFIA: 12
2.3 ENEO NA IDADI YA WATU: 12
2.4 MCHANGANUO WA WADAU 38
2.5 UCHAMBUZI WA HALI YA MANISPAA 39
2.5.1 UWEZO 39
2.5.2 UDHAIFU: 40
2.5.3 FURSA: 40
2.5.4 CHANGAMOTO KATIKA UTOAJI HUDUMA: 40
2.5.5 VIPAUMBELE VYA BAJETI YA 2016/2017 41
2.6 DIRA: 42
2.7 MADHUMUNI/DHAMIRA: 42
2.8 MALENGO NA MIKAKATI: 42
2.9 SERA NA MIKAKATI 50
2.10 UMBILE LA BAJETI 51
3 SURA YA 3: MATUMIZI YA KAWAIDA KWA FEDHA ZA VYANZO VYA NDANI .. **Error! Bookmark not defined.**
4 MATUMIZI YA KAWAIDA KWA FEDHA ZA RUZUKU – LOCAL GOVERNMENT BLOCK GRANT ..... **Error! Bookmark not defined.**
5 BAJETI YA MATUMIZI YA FEDHA ZA MFUKO WA PAMOJA - HEALTH SERVICE BASKET FUND ..... **Error! Bookmark not defined.**
6 BAJETI YA MIRADI YA MAENDELEO KWA VYANZO VYA NDANI (FOMU NA. 6) ..... **Error! Bookmark not defined.**
7 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA FEDHA ZA WADAU WA NDANI NA NJE **Error! Bookmark not defined.**
7.1 MIRADI YA MAENDELEO KWA FEDHA ZA WADAU WA NDANI ..... **Error! Bookmark not defined.**
7.1.1 FEDHA ZA KUTEKELEZA MIRADI YA MAENDELEO – LGDG – CAPACITY BUILDING (CBG) ..... **Error! Bookmark not defined.**
7.1.2 FEDHA ZA KUTEKELEZA MIRADI YA MAENDELEO – LGDG – CAPITAL DEVELOPMENT ..... **Error! Bookmark not defined.**
7.1.3 FEDHA ZA KUTEKELEZA MIRADI YA MFUKO WA JIMBO, ELIMU BURE (MSINGI NA SEKONDARI) - OTHER DEVELOPMENT GRANTS ..... **Error! Bookmark not defined.**
7.1.4 FEDHA ZA KUTEKELEZA MIRADI YA MAJI (RWSSP) - WORLD BANK .. **Error! Bookmark not defined.**
8 TAARIFA YA MISHAHARA MAENEO YA RUZUKU NA YASIYO YA RUZUKU **Error! Bookmark not defined.**
8.1 MUHTASARI WA WALIOMO NA WASIOKUWEMO KWENYE HATI YA MALIPO YA MISHAHARA – FOMU NA. 8A ..... **Error! Bookmark not defined.**
8.2 MUHTASARI KIFUNGU I, II, III – FOMU NA. 8B ..... **Error! Bookmark not defined.**
8.3 MUHTASARI WATUMISHI WALIOMO KWENYE HATI YA MALIPO – FOMU NA. 8C ..... **Error! Bookmark not defined.**
8.4 MUHTASARI WATUMISHI WASIOKUWEMO KWENYE HATI YA MALIPO – FOMU NA. 8D **Error! Bookmark not defined.**
8.5 MUHTASARI WA MAKISIO YA MISHAHARA – FOMU NA. 8E **Error! Bookmark not defined.**
8.6 WATUMISHI WANAOTARAJIA KUSTAAFU KWA MWAKA 2017/18 – FOMU NA. 8F ..... **Error! Bookmark not defined.**

9 MUHTASARI WA MAKISIO YA MISHAHARA – IKAMA NA UIMARA – FOMU NA. 9.....**Error! Bookmark not defined.**
10 UTARATIBU UNAOTUMIKA WAKATI WA KUCHAGUA MIRADI YA O & OD ITAKAYOTEKELEZWA KATIKA BAJETI NA MPANGO WA MUDA WA KATI (MTEF) 2017/2018 – 2019/20.....**Error! Bookmark not defined.**
11 MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA KATIKA KATA KWA BAJETI YA MWAKA 2017/2018 - HALMASHAURI YA WILAYA YA UBUNGO.....**Error! Bookmark not defined.**

MAJEDWALI YALIYOMO

JEDWALI 1: MAKADIRIO HALISI YA BAJETI YA 2016/17 NA MATUMIZI HADI 6
JEDWALI NA. 2: MUHTASARI WA BAJETI KWA MWAKA 2017/2018 6
JEDWALI NA. 3: MISHAHARA NA MATUMIZI YA KAWAIDA- FEDHA ZA RUZUKU ...7
JEDWALI NA. 4: RUZUKU YA MIRADI YA MAENDELEO 7
JEDWALI NA. 5: MAKISIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA KWA VYANZO VYOTE 2017/2018.....9
JEDWALI NA. 6: MAKISIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA VYANZO VYOTE MWAKA 2017/2018.....9
JEDWALI NA. 7: MAKISIO YA MATUMIZI YA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2017/2018 9
JEDWALI NA. 8: MCHANGANUO WA MATUMIZI YA MAPATO YA NDANI BAJETI YA MWAKA 2017/2018.....9
JEDWALI NA. 9: IDADI YA WATU KATIKA KATA 13
EDWALI NA. 10: HUDUMA ZA AFYA WILAYA YA UBUNGO.....20
JEDWALI NA. 11: MUHTASARI WA HALI YA MTANDAO WA BARABARA ZINAZOHUDUMIWA NA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO 22
JEDWALI NA. 12: MAKUNDI YA WADAU 39

MUHTASARI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2017/2018 NA MPANGO WA MUDA WA KATI 2017/2018 – 2019/2020

UTANGULIZI

Makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida na mpango wa maendeleo kwa mwaka **2017/2018 – 2019/2020** umeandaliwa kwa kuzingatia sera na miongozo ya Kitaifa, sheria ya bajeti Na 11 ya mwaka 2015, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Hotuba ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la 11 la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015 Malengo ya maendeleo endelevu, Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Mpango Mkakati Mpango wa tekeleza kwa matokeo makubwa sasa (BRN), Sera ya Taifa ya UKIMWI, Sera za kisekta, Mipango Shirikishi Jamii ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD) ya Kata na Mitaa. Aidha sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa sura ya 290 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2010 imezingatiwa.

BAJETI YA MWAKA 2017/2018

Katika mwaka wa fedha **2017/2018** Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inatarajia kukusanya/kupokea fedha kiasi cha **Tsh. 93,941,806,000.** Kati ya fedha hizo **Tsh. 70,685,171,000.00** ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu, **Tsh. 22,506,635,000.00** ni fedha za makusanyo ya ndani ya Halmashauri na **Tsh. 750,000,000.00** ni fedha za michango ya nguvu za wananchi.

RUZUKU ZA SERIKALI	MAPATOYA NDANI	MCHANGO YA WANANCHI	JUMLA
70,685,171,000	22,506,635,000	750,000,000	**93,941,806,000**
75%	**24%**	**1%**	**100%**

Kiasi cha **Tsh. 70,685,171,000.00** za ruzuku kutoka Serikali Kuu kinajumuisha kiasi cha **Tsh. 61,284,855,000.00** ikiwa ni mishahara, kiasi cha **Tsh.1,593,213,500.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, **Tsh. 7,807,102,500.00** fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo toka Serikali Kuu. Jumla ya **Tsh. 3,573,740,000.00** ni ruzuku kutoka mfuko wa matengenezo ya barabara - TAMISEMI (Road Fund).

Mpango huu umelenga katika kufikia dhima na dira ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

A) Huduma ya ukimwi kuboreshwa na maambukizi mapya kupunguzwa
B) Uboreshaji, uendelezaji na utekelezaji kikamilifu mpango wa Taifa wa kupambana na rushwa.
C) Kuimarika kwa upatikanaji na ubora wa huduma za jamii
D) Kuongezeka na kuboreka kwa huduma za kiuchumi na miundombinu
E) Kuimarika kwa utawala bora na utoaji wa huduma
F) Kuimarika kwa uwezo wa kiuchumi na kijinsia na ustawi wa jamii
G) Kuimarika kwa usimamizi wa kujikinga na maafa na milipuko ya magonjwa
H) Kuimarika kwa usimamizi wa maliasili na mazingira

- ## TAMKO LA MHESHIMIWA MSTAHIKI MEYA

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo katika kuboresha maisha ya wakazi wake, imeandaa mpango wa mwaka **2017/2018** na mpango wa muda wa kati **2017/2018** – **2019/2020** unaolenga kukuza uchumi, na kupunguza umaskini ili kufikia maendeleo endelevu ya kijamii, kiuchumi na kimazingira kwa wananchi wake. Mpango huu umezingatia sera na miongozo ya Kitaifa, sheria ya bajeti Na 11 ya mwaka 2015, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Hotuba ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la 11 la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015 Malengo ya maendeleo endelevu, Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Mpango Mkakati Mpango wa tekeleza kwa matokeo makubwa sasa (BRN), Sera ya Taifa ya UKIMWI, Sera za kisekta, Mipango Shirikishi Jamii ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD) ya Kata na Mitaa. Aidha sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa sura ya 290 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2010 imezingatiwa.

Aidha ili kutekeleza dhana nzima ya ugatuaji wa madaraka, mpango huu umeshirikisha jamii, katika mpango shirikishi ambao huanzia ngazi ya Mtaa. Hali hiyo imezingatia vipaumbele na mahitaji halisi ya wananchi katika maeneo yao. Mpango umejielekeza katika kutoa kipaumbele maeneo yanayoweza kutoa matokeo ya haraka (quick wins) ambayo yatasaidia ukuaji wa uchumi kwa haraka katika kipindi kifupi.

Aidha maeneo tuliyoyapa kipaumbele katika mpango huu ni pamoja na:-

I. Kuboresha na kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Manispaa.
II. Ujenzi wa ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.
III. Kuboresha miundombinu ya Afya, Shule za Msingi na Sekondari.
IV. Kuboresha miundombinu ya maji, masoko, barabara na Kilimo mjini.
V. Kuboresha hifadhi ya mazingira na ukusanyaji wa taka.

VI. Kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Ili kuyafikia mafanikio yaliyotajwa hapo juu, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo itasimamia yafuatayo:-

I. Kuimarisha mahusiano mazuri kati ya Serikali, mashirika yasiyo ya Kiserikali na wadau wengine.
II. Kuendelea kujenga uwezo na ujuzi kwa watumishi katika utoaji wa huduma zilizo bora na haraka.
III. Kuimarisha Utawala bora, Uwajibikaji na Uwazi.
IV. Kujenga uwezo kwa viongozi wakiwemo Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa katika kusimamia shughuli za wananchi.
V. Kushirikisha jamii katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo

Mpango wa muda wa Kati wa Matumizi na Bajeti ya mwaka **2017/2018** ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya **Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010 – 2015**. Hivyo matokeo ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti hii yameelekezwa katika kujibu matarajio ya watu ambayo ni utatuzi wa kero zao pamoja na maisha bora kwa kila Mtanzania.

MSTAHIKI MEYA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

- **MAELEZO YA MKURUGENZI WA MANISPAA**

Makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida na mpango wa maendeleo kwa mwaka **2017/2018 – 2019/2020** umeandaliwa kwa kuzingatia sera na miongozo ya Kitaifa, sheria ya bajeti Na 11 ya mwaka 2015, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Hotuba ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la 11 la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015 Malengo ya maendeleo endelevu, Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Mpango Mkakati Mpango wa tekeleza kwa matokeo makubwa sasa (BRN), Sera ya Taifa ya UKIMWI, Sera za kisekta, Mipango Shirikishi Jamii ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD) ya Kata na Mitaa. Aidha sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa sura ya 290 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2010 imezingatiwa.

MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2016/2017

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa mwaka **2016/2017** ilikadiria kutumia **Sh. 116,045,935,228.99** ikiwa ni pamoja na fedha za mfuko wa barabara. Kuanzia Julai hadi Disemba, 2016, Halmashauri ilikuwa imekusanya **Sh. 1,024,839,737.74** fedha za vyanzo vya ndani sawa na asilimia **8** ya maoteo ya **Tsh 13,300,416,090.50** vyanzo vya ndani yaliyotarajiwa kukusanywa kwa nusu mwaka wa bajeti na kutumia kiasi cha **Sh. 150,764,997.88.**Aidha mapato ya ndani yameanza kukusanywa mwezi novemba. Hadi sasa fedha za ruzuku hazijapokelewa kama inavyooneshwa katika Jedwali hapa chini.

JEDWALI 1: MAKADIRIO HALISI YA BAJETI YA 2016/17 NA MATUMIZI HADI DISEMBA, 2016

CHANZO CHA MAPATO KWA MWAKA 2016/2017	MAPATO YALIYOIDHINISHWA 2016/2017	MAPATO YALI-YOTOLEWA HADI DISEMBA 2016	MATUMIZI HADI DISEMBA 2016	ASILIMIA YA MATUMIZI
	1	2	3	(3/1)
A: FEDHA ZA NDANI				
(i) Mapokezi - Mishahara (PE)	1,027,080,000.00	0.00	0.00	0
(ii) Mapokezi – Matumizi (OC)	8,122,103,464.00	409,935,895.10	140,984,997.88	34
JUMLA NDOGO:	**9,149,183,464.00**	**409,935,895.10**	**140,984,997.88**	**3%**
B: FEDHA ZA RUZUKU				
(i) Mapokezi - Mishahara (PE)	48,663,242,400.00	0	0	0
(ii) Mapokezi – Matumizi (OC)	2,898,015,696.00	0	0	0
JUMLA NDOGO:	**51,561,258,096.00**	**0**	**0**	**0**
Ruzuku ya miradi	33,629,954,528.00	0	0	
Miradi kwa Fedha za Ndani	17,451,648,717.00	614,903,842.64	9,780,000.00	0
Mfuko wa barabara	4,233,546,143.00	0	0	0
Michango ya Wananchi	710,000,000.00	0	0	0
Jumla Ndogo	**56,025,149,388.00**	**614,903,842.64**		
JUMLA KUU	**116,735,590,948.00**	**1,024,839,737.74**	**150,764,997.88**	**13**

MAKISIO YA MATUMIZI KWA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

Katika mwaka wa fedha **2017/2018** Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inatarajia kukusanya/kupokea fedha kiasi cha **Tsh. 93,941,806,000.** Kati ya fedha hizo **Tsh. 70,685,171,000.00** ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu, **Tsh. 22,506,635,000.00** ni fedha za makusanyo ya ndani ya Halmashauri na **Tsh. 750,000,000.00** ni fedha za michango ya nguvu za wananchi.

Kiasi cha **Tsh. 70,685,171,000.00** za ruzuku kutoka Serikali Kuu kinajumuisha kiasi cha **Tsh. 61,284,855,000.00** ikiwa ni mishahara, kiasi cha **Tsh.1,593,213,500.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, **Tsh.7,807,102,500.00** fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo toka Serikali Kuu. Angalia jedwali hapo chini;

JEDWALI NA. 2: MUHTASARI WA BAJETI KWA MWAKA 2017/2018

RUZUKU ZA SERIKALI	MAPATOYA NDANI	MCHANGO YA WANANCHI	JUMLA
70,685,171,000	22,506,635,000	750,000,000	**93,941,806,000**

75%	**24%**	**1%**	**100%**

JEDWALI NA. 3: MISHAHARA NA MATUMIZI YA KAWAIDA- FEDHA ZA RUZUKU

KASMA	IDARA/KITENGO	MISHAHARA	MATUMIZI YA KAWAIDA	JUMLA
5000	UTAWALA	0	40,656,000.00	40,656,000.00
5000	USHIRIKA	0	4,716,500.00	4,716,500.00
5003	UKAGUZI WA NDANI	0	4,129,500.00	4,129,500.00
5005	MIPANGO	0	8,186,000.00	8,186,000.00
5004	GS 2 & ABOVE	3,325,830,400.00	0	3,325,830,400.00
5006	ELIMU MSINGI	29,872,836,600.00	721,969,000.00	30,594,805,600.00
5008	ELIMU SEKONDARI	15,650,620,000.00	550,342,500.00	16,200,962,500.00
5009	AFYA	10,257,136,000.00	205,920,000.00	10,463,056,000.00
5014	UJENZI	525,636,000.00	15,732,000.00	541,368,000.00
5017	MAJI	209,544,000.00	31,503,000.00	241,047,000.00
5032	MISHAHARA WATENDAJI WA MITAA (MEOs PE)	598,512,000.00	0	598,512,000.00
5033	KILIMO	379,560,000.00	5,029,500.00	384,589,500.00
5034	MIFUGO	465,180,000.00	5,029,500.00	470,209,500.00
	TOTAL PE & OC	**61,284,855,000.00**	**1,593,213,500.00**	**62,878,068,500.00**

JEDWALI NA. 4: RUZUKU YA MIRADI YA MAENDELEO

NAMBA YA MRADI	CHANZO CHA FEDHA	RUZUKU YA MAENDELEO (NDANI)	RUZUKU YA MAENDELEO (NNJE)	JUMLA
5010	MFUKO WA AFYA WA PAMOJA (HSBF)	-	1,846,377,000.00	1,846,377,000.00
	RUZUKU YA UJENZI WA OFISI ZA HALMASHAURI	1,500,000,000.00	-	1,500,000,000.00
6277	RUZUKU YA MAENDELEO YA MIRADI NA KUJENGA UWEZO(LGDG)	2,812,949,000.00	-	2,812,949,000.00
4322	PROGRAMU YA ELIMU BURE SHULE ZA MSINGI	620,444,000.00	-	620,444,000.00

3280	RURAL WATER SUPPLY AND SANITATION PROGRAMME (RWSSP)	-	179,962,500.00	179,962,500.00
4393	PROGRAMU YA ELIMU BURE SHULE ZA SEKONDARI	718,736,000.00	-	718,736,000.00
	MFUKO WA JIMBO	128,634,000.00	-	128,634,000.00
	JUMLA	**5,780,763,000.00**	**2,026,339,500.00**	**7,807,102,500.00**

MAKISIO YA MATUMIZI KWA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

Katika mwaka wa fedha **2017/2018** Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inatarajia kutumia fedha kiasi cha **Tsh. 93,941,806,000.00.** Kati ya fedha hizo **Tsh. 71,880,722,500.00** ni matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na asilimia **77** ya bajeti yote na **Tsh. 22,061,083,500.00** ni fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia **23** ya bajeti. Angalia jedwali namba 7.

JEDWALI NA. 5: MAKISIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA KWA VYANZO VYOTE 2017/2018

CHANZO CHA FEDHA	MATUMIZI YA KAWAIDA (PE & OC)	MIRADI YA MAENDELEO	JUMLA
VYANZO VYA NDANI	9,002,654,000.00	13,503,981,000.00	22,506,635,000.00
RUZUKU YA SERIKALI KUU	62,878,068,500.00	7,807,102,500.00	70,685,171,000.00
MICHANGO YA WANANCHI	-	750,000,000.00	750,000,000.00
JUMLA	**71,880,722,500.00**	**22,061,083,500.00**	**93,941,806,000.00**
ASILIMIA	**77**	**23**	**100**

JEDWALI NA. 6: MAKISIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA VYANZO VYOTE MWAKA 2017/2018

MGAWANYO	VYANZO VYA NDANI	RUZUKU YA SERIKALI KUU	JUMLA
MISHAHARA	658,644,000.00	61,284,855,000.00	61,943,499,000.00
MATUMIZI YA KAWAIDA	8,344,010,000.00	1,593,213,500.00	9,937,223,500.00
MATUMIZI YA KAWAIDA (COST SHARING)	749,460,000.00	0.00	749,460,000.00
JUMLA	**9,002,654,000.00**	**62,878,068,500.00**	**71,880,722,500.00**
ASILIMIA	**13%**	**87%**	**100%**

JEDWALI NA. 7: MAKISIO YA MATUMIZI YA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2017/2018

CHANZO CHA FEDHA ZA MIRADI	ADA YA UCHANGIAJI (COST SHARING)	VYANZO VYA NDANI	MCHANGO WA WANANCHI	RUZUKU YA SERIKALI	JUMLA
THAMANI	1,086,000,000	12,417,981,000	750,000,000	7,807,102,500	**22,061,083,500**
ASILIMIA	**5%**	**56%**	**3%**	**35%**	**100%**

JEDWALI NA. 8: MCHANGANUO WA MATUMIZI YA MAPATO YA NDANI BAJETI YA MWAKA 2017/2018

CHANZO CHA FEDHA	MIRADI YA MAENDELEO	MATUMIZI YA KAWAIDA	MISHAHARA	JUMLA
VYANZO VYA NDANI	13,503,981,000.00	8,344,010,000.00	658,644,000.00	**22,506,635,000.00**
ASILIMIA	**60**	**37**	**3**	**100**

Aidha Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imetimiza vigezo vya kutenga asilimia 60 ya mapato ya ndani kutumika katika miradi ya maendeleo. Hivyo jumla ya **Tsh. 13,503,981,000.00** sawa na asilimia **60** ya bajeti ya makusanyo ya ndani imetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. (Angalia jedwali namba 10).

Bajeti hii imelenga katika kuboresha maisha ya wananchi na kukuza kipato cha mkazi ili kukuza uchumi wetu wa ndani. Vipaumbele vitakuwa katika maeneo yafuatayo:-

i. Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.
ii. Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi kwa kujenga jengo la utawala la Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo Luguruni – Kwembe, kununua vitendea kazi na kutoa stahiki kwa watumishi na waheshimiwa madiwani.Jumla ya **Tsh. 6.3 billion** zimetengwa.
iii. Kuboresha miundombinu ya barabara kwa kujenga Madaraja/ Makalvati, barabara kwa kiwango cha lami, kufanya matengenezo ya kawaida ya barabara, muda maalum, maeneo korofi, njia za waenda kwa miguu, Ujenzi wa Mifereji katika barabara za Manispaa. Jumla ya **Tsh 6.3 bilion** zimetengwa

iv. Kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa kununua madawa na vifaa tiba na kuboresha miundo mbinu ya afya .Jumla ya **Tsh.5.7 billion** zimetengwa.
v. Kuboresha miundo mbinu ya shule za Msingi na Sekondari kwa kununua madawati, kujenga madarasa, vyoo, nyumba za walimu, maabara na ukarabati wa miundombinu. Jumla ya **Tsh.5.2 billion** zimetengwa
vi. Kuboresha usafi wa mazingira na na ukusanyaji taka na kununua magari makubwa ya taka Jumla ya **Tsh.1.3 billion** zimetengwa.

vii. Kutoa mikopo kwa wajasiliamali wa dogo kwa vikundi vya wanawake na vijana ili kuongeza ajira na kukuza kipato cha Mkazi.Jumla ya **Tsh.1.2 billion** zimetengwa

viii. Kununua magari na mitambo ;magari 6 ya ofisi, gari moja la maji machafu na gari 1 la maji safi, jenereta. Jumla ya **Tsh 1.1 billion** zimetengwa.

ix. Kulipa fidia kupisha ujenzi wa miradi mabali mbali ya maendeleo. Jumla ya **Tsh.1 billion** zimetengwa .

x. Kuboresha upatikana maji safi na salama kwa wakazi wa Ubungo kwa kujenga na kukarabati miundo mbinu ya maji. Jumla ya **Tsh.561 million** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji

xi. Mipango miji na upimaji. Jumla ya **Tsh.550 million** zimetengwa

Nawasilisha.

John L. Kayombo
MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

SURA YA KWANZA: UCHAMBUZI WA KIMAZINGIRA

TASWIRA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ni moja kati ya Halmashauri 6 za Mkoa wa Dar es Salaam ambazo zinaunda Mkoa wa Dar es Salaam, Zingine ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Ilala, Temeke, Kigamboni na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo ilianzishwa kwa Sheria ya Serikali (Mamlaka ya Mji) sura ya 288 kupitia (Government Notice No. 4) ya mwaka 2000 na Ofisi ya Raisi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kama chombo huru, hivyo kuipa mamlaka ya kuongeza ubora wa utoaji wa huduma kwa wananchi wake.

MAHALI ILIPO NA MUONEKANO WA KIJIOGRAFIA:

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inapakana na Wilaya ya Kibaha kwa upande wa Kaskazini, Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni kwa upande wa Kusini-Mashariki, Wilaya ya Kisarawe kwa upande wa Magharibi. Halmashauri inaunganishwa na sehemu nyingine za miji na nchi kwa mtandao wa barabara na mawasiliano. Barabara kuu ni pamoja na barabara ya Morogoro, Mandela, barabara ya Sam Nujoma.

ENEO NA IDADI YA WATU:

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina ukubwa wa kilomita za mraba **210** Kwa mujibu wa Sensa ya Taifa ya idadi ya watu na makazi ya mwaka **2012,** Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ilikuwa na idadi ya watu wapatao **845,368** ambapo wanaume ni **409,149** na wanawake ni **436,219.** Kutokana na ongezeko la ukuaji wa idadi ya watu ya asilimia **5.0** kwa mwaka, Manispaa inakadiriwa kuwa na idadi ya watu wapatao **1,078,928** ifikapo mwaka **2017,** hivyo kila kilometa ya mraba kuwa na ujazo wa watu **5,138.**

UTAWALA

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imegawanyika katika kata 14 na Mitaa 91.

JEDWALI NA. 9: IDADI YA WATU KATIKA KATA

S/N	KATA	IDADI YA WATU KWA JINSI 2012			IDADI YA WATU KWA JINSI 2016		
		ME	KE	JUMLA	ME	KE	JUMLA
1	Mburahati	16,784	17,339	34,123	21,421	22,129	43,550
2	Sinza	18,892	21,654	40,546	24,112	27,637	51,749
3	Makuburi	28,021	29,387	57,408	35,763	37,506	73,269
4	Mabibo	41,824	43,911	85,735	53,379	56,043	109,422
5	Manzese	34,495	36,012	70,507	44,025	45,961	89,986
6	Ubungo	27,221	28,794	56,015	34,742	36,749	71,491
7	Makurumla	30,933	32,419	63,352	39,479	41,376	80,855
8	Mbezi	35,637	37,777	73,414	45,483	48,214	93,697
9	Msigani	26,479	28,632	55,111	33,795	36,542	70,337
10	Kimara	36,654	39,923	76,577	46,781	50,953	97,734
11	Saranga	49,263	54,864	104,127	62,873	70,022	132,895
12	Goba	21,066	21,603	42,669	26,886	27,572	54,458
13	Kibamba	13,840	15,045	28,885	17,664	19,202	36,866
14	Kwembe	28,040	28,859	56,899	35,787	36,832	72,619
	TOTAL	**409,149**	**436,219**	**845,368**	**522,190**	**556,738**	**1,078,928**

Chanzo: Sensa ya Taifa ya Idadi ya Watu na Makazi 2012
Angalizo: Makisio ya idadi ya Watu; mwaka wa sensa 2012, ongezeko kwa mwaka 5.0%

SHUGHULI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo Inakadiriwa kuwa na idadi ya wakazi **733,671** wenye uwezo wa kufanya kazi ambapo **61%** wameajiriwa sekta binafsi, **35%** wamejiajiri wenyewe na **4%** wameajiriwa katika sekta ya umma. Shughuli zinazofanywa na wakazi wenye uwezo wa kufanya kazi ni kampuni binafsi, taasisi, biashara. Wengine wanajishughulisha katika biashara ndogo ndogo, ufugaji na Kilimo cha mjini.

HUDUMA ZA KIUCHUMI NA KIJAMII KATIKA MANISPAA

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imejikita katika kutoa huduma za kiuchumi na kijamii kwa kuzingatia sera na miongozo ya Taifa na vipaumbele vya kisekta.

ELIMU YA MSINGI

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina jumla ya shule za awali **113** kati ya shule hizi, shule za Serikali ni **60** na zisizo za Serikali ni **53**. Pia Halmashauri ina jumla ya Shule za Msingi **113**, ambapo shule za Serikali ni **64** na zisizo za Serikali ni **49**.

Shule **113** za Msingi za Serikali zina jumla ya wanafunzi **76,346** kuanzia darasa la kwanza hadi la Saba na walimu **2,434**. Miundombinu ya shule iliyopo ni pamoja na vyumba vya madarasa **833**, madawati **17,121** na matundu ya vyoo kwa wanafunzi wa kawaida **710**, maktaba **8** na nyumba za walimu **112**. Aidha, kuna madarasa **9** ya MEMKWA yenye jumla ya wanafunzi **340** katika Shule za Msingi, MUKEJA (Mpango wa Uwiano kati ya Elimu ya watu wazima na Jamii) ina vituo 2 na wanakisomo 192,PESH (Elimu ya Sekondari huria) ina vituo 2 na wanafunzi 850, ODL (Elimu kwa njia ya masafa) ina vituo 4 na wanafunzi 222. PROGRAM ya Ndio NAWEZA ina vituo 13 na wanafunzi 99, VITUO VYA UFUNDI STADI, vina wanafunzi 129. Halmashauri pia Ina shule maalum **1** na vitengo **13** vya Elimu Jumuishi (Inclusive Education) vyenye wanafunzi **1,507** na Walimu **48.**

Jedwali kuonyesha idadi ya walimu kwa taaluma zao.

KIWANGO CHA ELIMU	Walimu wenye ajira ya Kudumu (Permanent)		
	Me	Ke	Jumla
Shahada ya Uzamili (Masters)	2	21	26
Shahada (Degree)	104	259	363
Stashahada (Diploma)	104	315	419
Daraja A (Cheti)	346	1,343	1,589
Wengineo	2	35	37
JUMLA KUU	**558**	**1,973**	**2,434**

Changamoto

- Upungufu wa vyumba vya madarasa **942**
- Upungufu wa vyoo vya wanafunzi wa kawaida na walimu **2,918**
- Upungufu wa vyoo rafiki vya Walemavu **22**
- Upungufu wa nyumba za walimu **1,871**
- Upungufu wa madawati **11,312**
- Miundo mbinu iliyopo mingi inahitaji ukarabati.
- Shule **18** kati ya **64** za serikali hazina huduma ya maji kwa kipindi chote cha mwaka.
- Shule **35** kati ya **64** za serikali hazina huduma ya umeme.
- Shule **61** kati ya **64** za serikali hazina huduma ya kompyuta
- Madai mbalimbali ya watumishi wa Idara ya Elimu kutolipwa kwa wakati. Madai hayo ni kama yafuatayo; nauli za likizo, malimbikizo ya mishahara, honoraria kwa wawezeshaji wa MEMKWA na MUKEJA
- Watumishi kutopatiwa mafunzo Eendelevu kazini ili kuongeza ufanisi kazini.
- Walimu wengi kuwiwa kujiendeleza katika fani tofauti na elimu na baada ya kujiendeleza kutokuwa na ari ya kufundisha na kutafuta kazi tofauti na Ualimu.
- Kukosekana kwa Walimu mahiri kwa masomo ya Hisabati, Sayansi na Kiingereza

Mikakati ya kuondoa changamoto:

- Kushawishi wananchi kuchangia huduma za elimu.
- Halmashauri itumie vyanzo vya ndani kuboresha miundo mbinu ya shule.
- Serikali kuchangia ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu vyoo vya wanafunzi, ununuzi wa madawati na ukarabati wa miundo mbinu chakavu.
- Kushirikisha wadau mbalimbali kama vile mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) kuchangia kuboresha miundombinu.

- Mkoa umeunda timu ya kuandaa mkakati wa kutengeneza madawati ya shule zote za Mkoa wa Dar es Salaam.
- Kuhakikisha kila Shule ina darasa la Elimu ya Awali.
- Kuhakikisha mazoezi ya kutosha ya mitihani yanatolewa mara kwa mara. Kwa mfano; mitihani ya wiki, mitihani ya Mock ya Kata, Wilaya na Mkoa.
- Kubaini idadi ya watoto wasiojua kusoma na kuandika katika kila shule hivyo kuanzisha mpango wa kuwasaidia.
- Kuhimiza utoaji wa chakula shuleni kwa wanafunzi hususani uji.
- Kuhakikisha masomo yote yanapewa uzito sawa katika ufundishaji.
- Kuendesha Semina Elekezi Kwa walimu wote wa masomo mbali mbali pamoja na wakuu wa shule.
- Kutembelea shule na kufanya ukaguzi ili kugundua mapungufu na kurekebisha kasoro zinazojitokeza.
- Kusimamia michezo ya Umitashumta kuanzia ngazi ya kata hadi ngazi ya Taifa ili kuinua vipaji vya wanafunzi.
- Kuboresha miundombinu ya shule kwa kujenga vyoo, madarasa na nyumba za walimu kulingana na fedha zinazopatikana kutoka S/KUU.

ELIMU YA SEKONDARI:

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo na Jumla ya shule za Sekondari **66** ikiwa shule za Serikali ni **27** na za binafsi ni **39**. Kati ya shule za Serikali **27** tulizojenga wenyewe, shule **8** ni za mjini na shule **19** ni za vijijini. Pia shule za Serikali zina jumla ya walimu **955** kati yao walimu wakiume ni **296** na wakike ni **659**, na wanafunzi walliopo ni **10,849.**

HALI YA WALIMU

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina jumla ya walimu **955** wenye viwango tofauti vya elimu kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo;

Jedwali linaloonyesha idadi ya walimu kwa taaluma zao

S/N	Taaluma	WANAUME	WANAWAKE	JUMLA
1	Shahada yauzamivu (phd)	0	0	0
2	Shahada yauzamili (masters)	6	19	25
3	Shahada (bachelor)	160	359	519
4	Diploma	123	277	400
5	Leseni	7	4	11
	JUMLA	**296**	**659**	**955**

Kutokana na idadi ya wanafunzi waliopo katika shule zetu za sekondari idara ina upungufu wa walimu **263** katika masomo yafuatayo;

S/NO	SOMO	MAHITAJI	WALIOPO	UPUNGUFU
1	Hisabati	136	67	69
2	Fizikia	95	45	50
3	Kemia	86	54	32
4	Bailojia	115	65	50
5	Kompyuta	-	-	0
6	Commerce	46	19	27
7	B/keeping	48	17	31
8	Kifaransa	7	3	4
JUMLA		**533**	**270**	263

HAALI YA MIUNDOMBINU ELIMU SEKONDARI

S/NO	AINA	MAHITAJI	YALIYOPO	UPUNGUFU
1	MADARASA	569	429	140
2	MADAWATI	21,667	15,567	6100
3	MAABARA	100	63	37
4	VYOO	1,257	385	872
5	NYUMBA ZA WALIMU	822	10	812
6	STOO	42	4	38
7	MAKTABA	32	2	30
8	JENGO LA UTAWALA	29	3	26
9	OFISI ZA WALIMU	85	5	80

IDARA YA UTAWALA

Idara hii ni moja ya idara inayoshughulikia maslahi ya wafanyakazi yenye jumla ya wafanyakazi 4,450 kutoka idara mbalimbali.

MAJUKUMU YA IDARA YA UTAWALA

- Kushugulikia ajira na vyeo vya watumishi.
- Kuratibu shughuli za Mafunzo kwa watumishi.
- Kuratibu dawati la malalamiko.
- Kushughulikia Mikopo kwa watumishi katika taasisi za kifedha
- Kushughulikia maslahi mbalimbali ya watumishi.
- Kuandaa bajeti ya Mishahara (PE)
- Kuingiza na kurekebisha taarifa mbalimbali za watumishi kwenye mfumo wa taarifa za utumishi (HCIMS).
- Kusimamia zoezi la upimaji utendaji kazi (OPRAS)
- Kusimamia ikama na Tange ya watumishi wote.
- Kuratibu Mashauri ya nidhamu kwa watumishi.
- Kuratibu shughuli za vikao na mikutano.
- Kuratibu shughuli za kata na mitaa.
- Kuratibu maslahi ya viongozi wa kuchaguliwa (Madiwani).

CHANGAMOTO

- Upungufu wa Ofisi kulingana na idadi ya watumishi waliopo.
- Bajeti kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi (Fedha za Halmashauri) haitoshi.
- Fedha za kujenga uwezo kutoka Serikali kuu (CBG) kutofika kabisa wakati zinatengewa shughuli kwa ajili ya utekelezaji katika mwaka husuka.

MIKAKATI

- Kuna mpango wa kujenga Ofisi mpya.
- Kuondoa utegemezi wa fedha za CBG kwa kuongeza bajeti ya fedha za ndani

IDARA YA FEDHA NA BIASHARA

Idara hii inahusika na kulinda, kuziendeleza, kuhakikisha matumizi mazuri ya mali za Halmshauri. Aidha idara ya fedha na biashara inahakikisha thamani ya fedha kwa miradi na shughuli zote za kawaida za uchumi, biashara fedha/Mali za Halmashauri.

MAJUKUMU YA IDARA FEDHA NA BIASHARA

- Kuhakikisha makusanyo na matumizi yote ya Halmsahuri yanafanyika kwa kuzingatia sharia taratibu na kanuni za fedha.
- Kushauri katika masuala yaote ya yanayohusu fedha na uwekezaji katika Halmashauri ili kuleta tija stahiki.
- Kutoa taarifa zote za fedha na bishara za Halmashauri kwa wadau mbalimbali wa taarifa.
- Kulinda na kuhifadhi mali zote za halmshauri kitaalamu.
- Kuhakikisha kuna thamani ya fedha katika matumizi yote yanayofanywa na Halmashauri.
- Kukusanya na kutumia kodi, na shuru zote za Halmashauri.

CHANGAMOTO

- Upungufu wa Ofisi kulingana na idadi ya watumishi waliopo.
- Bajeti kwa ajili ya Kununa vitendea kazi ikiwamo mifumo ya kielektroniki,magari,magari,kujenga uwezo kwa watumishi haitoshi
- Maagizo ya serikali kutumia mifumokatika kufanya makusanyo na kutumia fedha za serikali ilhali bado miundombinu stahiki katika sehemu mbalimbali za kiutawala hauja tengeamaa.

MIKAKATI

- Kuna kujenga, kununua na kuboresha mifumo na miundombinu stahiki kwa awamu katika ngazi mbalimbali za kiutawala kuanza na makao makuu, kata, mtaa, masoko, hospitali, vituo vya afya n. k
- Kuanzishwa vituo maalumu vya kukusanya mapato kwa kuangalia walipakodi ili kupunguza adha ya kulipa kodi.

- Kuondokana na matumizi ya mkono katika kukusanya na kufanya malipo ya serikali na badala yake shughuli zote hizikuwa katika mfumo kwenye ngazi zote za kiutawala za serikali.

IDARA YA AFYA

Hospitali ya **Sinza** inatoa huduma za Afya katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ikiwa kama hospitali za wilaya, zahanati **16** za serikali zimeendelea kuhudumia jamii ya Ubungo . Huduma ya Afya katika vituo hivi hutolewa kwa nia ya kuboresha tiba na kinga za magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

EDWALI NA. 10: HUDUMA ZA AFYA WILAYA YA UBUNGO

Huduma	Umiliki		Jumla
	Serikali	Binafsi	
Hospitali	1	4	5
Vituo vya Afya	0	6	6
Zahanati	16	41	57
Jumla	**17**	**51**	**68**

Hospitali ya Wilaya inahudumia wagonjwa kati ya **1,000** hadi **1,500** kwa siku.

USAFISHAJI NA MAZINGIRA

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuboresha usafi wa mazingira kwa kuzingatia maeneo ya udhibiti wa taka ngumu, udhibiti wa maji taka, uelimishaji na uhamasishaji wa jamii ili iweze kushiriki vyema katika usafishaji mazingira yanayowazunguka, utafiti na uendelezaji wa teknolojia kutumia taka kama malighafi (Composting/Recycling/Reuse), upendezeshaji Manispaa (beautification).

Katika kukabiliana na tatizo la uchafuzi wa mazingira, Halmashauri inatekeleza mkakati wa kuboresha usafi kwa kuwashirikisha wadau wote wa Manispaa ya Kinondoni. Lengo kuu la kuwashirikisha wadau wote ni kwamba Halmashauri pekee yake haina uwezo wa kugharamia shughuli zote za usafi

na hasa kwa kuzingatia gharama zinazohitajika katika kutoa huduma hiyo. Nia ya mabadiliko haya ni kuboresha na kudumisha hali ya utoaji wa huduma za uzoaji taka na wananchi kushiriki katika kuchangia gharama za uendeshaji.

Changamoto:-

- Uwezo mdogo wa kudhibiti taka kulinganisha na kiasi kinachozalishwa.
- Ukosefu wa zana za kisasa za kutosha za kudhibiti taka.
- Umbali wa kufika dampo unaosababisha gharama kubwa ya mafuta ya magari ya taka.

BARABARA

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina jumla ya barabara zenye urefu wa kilometa **409.4**. Kati ya hizo barabara zenye urefu wa kilometa **23.1** zinamilikiwa na kuhudumiwa na TANROADS na barabara zenye urefu wa kilometa **386.3** zinamilikiwa na kuhudumiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Katika barabara zinazohudumiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kilometa **19.25** ni za kiwango cha lami, kilometa **245.25** ni za kiwango cha changarawe na kilometa **118.05** ni za kiwango cha udongo.

Hali ya barabara za Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo si nzuri sana kwa kuwa nyingi ni za changarawe na pindi zinapofanyiwa matengenezo ya kawaida na ya mara kwa mara hupokea magari mengi na kuharibika haraka. Kwa wastani ni asilimia **29.25** tu ya barabara za lami na changarawe ndio zipo katika hali nzuri na ya wastani kama inavyoonekana katika Jedwali hapa chini.

JEDWALI NA. 11: MUHTASARI WA HALI YA MTANDAO WA BARABARA ZINAZOHUDUMIWA NA HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

JUMLA YA UREFU (km)	KIWANGO CHA LAMI			KIWANGO CHA CHANGARAWE			KIWANGO CHA UDONGO		
386.3	Nzuri (Km)	Wastani (Km)	Mbaya (Km)	Nzuri (Km)	Wastani (Km)	Mbaya (Km)	Nzuri (Km)	Wastani (Km)	Mbaya (Km)
	19.25	0.0	3.75	82.85	107.45	54.95	10.9	46.3	60.85
Jumla (km)	23.0			245.25			118.05		

CHANGAMOTO

1. Kuongezeka kwa wingi wa magari barabarani na hivyo kusababisha msongamano wa magari katika barabara kuu za Manispaa.
2. Uwezo mdogo wa Manispaa wa kujenga barabara zake kutoka kiwango cha changarawe na kuwa za lami.
3. Kuwa na bajeti ndogo ya matengenezo ya kawaida ya barabara za Manispaa kutoka mifuko mbalimbali ya fedha.
4. Ujenzi wa magorofa unaoendelea kwa kasi unaongeza uharibifu wa haraka kwa barabara mara zinapotengenezwa kwa kuwa zinapitisha uzito mkubwa wa vifaa vya ujenzi.
5. Ukosefu wa maabara ya manispaa inayotumika kupima ubora wa kazi za ujenzi.

MIKAKATI

1. Manispaa itaendelea kutenga fedha za kujenga barabara kwa kiwango cha lami katika bajeti zake ili kuweza kuboresha urefu wa mtandao wa barabara na hatimaye kuweza kupunguza msongamano wa magari.
2. Kushawishi wananchi na sekta binafsi kuchangia ujenzi wa barabara za lami kwenye maeneo yao.
3. Kuendelea kushawishi **TAMISEMI** waongeze bajeti ya matengenezo ya barabara kupitia Mfuko wa Barabara.
4. Kushawishi TAMISEMI kutenga fedha maalumu kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Lami katika Manispaa.
5. Kuendelea kuwashawishi wananchi kuchangia mafuta katika greda la Manispaa ili kuweza kuchonga barabara za mitaa yanayoishi.

SEKTA YA MAJI

Huduma ya maji kwa wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, kwa kiasi kikubwa hutolewa na Mamlaka ya Maji ya Mjini Dar es Salaam (DAWASA) ambayo imekodisha shughuli za utoaji huduma kwa kampuni ya DAWASCO.

Maji yanayozalishwa yanakidhi mahitaji kwa asilimia 68. Upungufu wa maji unasababishwa na uwezo mdogo wa vyanzo vya maji vya miradi ya maji ambayo ilijengwa mwaka 1940 na 1976 wakati huo idadi ya wakazi wa jiji ilikuwa ni ndogo. Miradi ya upanuzi wa vyanzo wa maji inayojengwa na DAWASA itaongeza ujazo wa uzalishaji maji hivyo kupunguza upungufu wa maji kwa asilimia 85% kwa jiji la Dar es Salaam. Maeneo yasiyohudumiwa na Mtandao wa DAWASA hupata maji kutoka Miradi inayoendeshwa na Taasisi, Sekta binafsi na Jumuiya za watumia maji, chanzo kikubwa cha maji haya ni visima vifupi na virefu. Katika Manispaa yetu ya Ubungo kuna visima 119 vinavyomilikiwa na Manispaa. Aidha kuna visima vya taasisi na watu binafsi visivyopungua 600 katika maeneo mbalimbali ya Manispaa, Malengo ya Kitaifa ni kuwapatia wakazi wa Mijini maji kwa asilimia 90 na asilimia 100% ifikapo 2025.

Pamoja na juhudi za DAWASA, kuna miradi ya maji inayotekelezwa na Halmashauri ya Manispaa Ubungo kupitia wadau mbalimbali wa maji ikiwemo; Ujenzi wa miradi ya maji ya(Programu ya maji na Usafi wa Mazingira Vijijini) imejengwa katika maeneo ya Mpiji Magohe na Kibwegere (RWSSP) Kazi ya ujenzi imekamilika na miradi imekabidhiwa kwa jumuiya za watumiaji maji kwa lengo la kuendesha na kusimamia miradi ya maji. Manispaa inaendelea na Ujenzi wa mradi wa maji katika kata ya Kwembe mtaaa wa Kingazi A pamoja na kufanya upanuzi wa mradi wa maji katika kata ya mbezi. Aidha kuna mradi wa maji na usafi wa mazingira (Maji yetu) ambao umefadhiliwa na jumuia ya Ulaya, Serikali ya Ubelgiji na Serikali ya Tanzania. Mradi huu unatekelezwa katika Kata za Kwembe, Kibamba na Mburahati. Utekelezaji wa Mradi huu katika kata ya Mburahati, Kibamba na Kwembe miradi imekamilika na imekabidhiwa kwa jamiii. Pia Kupitia mradi wa BTC mafunzo yametolewa katika kamati 3 za maji maeneo ya Kwembe, Mburahati na Kibamba juu ya utunzaji wa mifuko ya maji pamoja na miradi ya madare kisauke,Mabwepande.

CHANGAMOTO ZINAZOKABILI SEKTA YA MAJI:

Sekta ya maji katika Manispaa ya Ubungo inakabiliwa na changamonto nyingi kama ifuatavyo:-

i) Uwezo mdogo wa vyanzo vya maji vilivyokwishabainishwa,

ii) Uzalishaji mdogo wa maji katika visima vya maji vyenye uwezo mkubwa,

iii) Upotevu wa maji mengi katika mtandao wa mabomba ya kusafirisha na kusambaza maji,

iv) Watumiaji kutokulipia ankara za maji,

v) Gharama kubwa za miundombinu ya maji,

vi) Uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji,

vii) Uharibifu wa miundombinu,

x) Elimu duni ya afya, usafi wa mazingira na uendeshaji miradi.

xi) Uwezo mdogo wa kamati za maji katika kusimamia miradi ya maji hususani mapato yatokanayo na mauzo ya Maji.

xii) Ubadilishaji wa kamati za maji mara kwa mara (uongozi wa jumuiya ya watumia maji)kabla ya kumaliza muda wake.

MIKAKATI YA KUBORESHA HUDUMA YA MAJI KATIKA HALMASHAURI

i) Kuunda vyombo vya watumia maji ili wananchi waweze kusimamia na kuendesha miradi yao ya maji katika ngazi ya Jamii.

ii) Kusajili vyombo vya watumiaji maji

iii) Kushirikiana na Wadau mbalimbali ili kuweza kupata fedha na kutekeleza Miradi mikubwa ya maji ya kuwahudumia jamii.

iv) Kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali juu ya hifadhi ya mazingira na uendeshaji wa miradi ya Maji hususani ngazi ya Jamii.

v) Kushirikisha Sekta binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa huduma ya maji katika ngazi zote.

vi) Kushirikiana na DAWASA katika utekelezaji wa mpango wa muda mrefu wa kuboresha vyanzo vya maji vilivyopo ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa vyanzo vipya vya maji

MAFANIKIO YA SEKTA YA MAJI

i) Kukamilika kwa ujenzi wa miradi ya Mpiji Magohe na Kibwegere (RWSSP) Kazi ya ujenzi na kukabidhiwa kwa jumuiya za watumiaji maji kwa lengo la kuendesha na kusimamia miradi ya maji.
ii) Kukamilika kwa mradi wa Mburahati,Kibamba na Kwembe (Maji yetu) uliyofadhiliwa na jumuia ya Ulaya, Serikali ya Ubelgiji na Serikali ya Tanzania.
iii) Kukamilika kwa upanuzi wa mradi wa maji kwa ulazaji wa bomba kwa umbali wa 1.2 km katika kata ya Mbezi.
iv) Kukamilika kwa mradi wa maji wa kisima cha maji katika kata ya kwembe mtaa wa kingazi A
v) Uendelezaji wa visima vya maji katika kata ya Kigogo .
vi) Usajili wa vyombo vya watumiaji maji 3 katika Halmashauri umefanyikaji
vii) Utoaji wa elimu juu ya usafi wa mazingira katika kamati za maji 6 umefanyika.

SEKTA YA KILIMO

Eneo lenye ukubwa wa **Ha 1,850** kinafaa kwa shughuli za kilimo. Ingawa takwimu zinaweza kubadilia kwa sababu ya upanuzi wa maeneo kwa shughuli zisizo za kilimo. Makadirio ya ukubwa wa eneo linalozalishwa mazao ya chakula na biashara ni **174.94 Ha** ambapo ni sawa na asilimia **9.45%** ya kiasi cha eneo linalofaa kwa shughuli za kilimo. Wakulima wanajihusisha na kilimo cha biashara (kiasi kikubwa) na kaisi kidogo na wengi wao hutumia zana zisizo na ubora hasa jembe la mkono. Wachache kati yao hutumia zana zilizo bora kama matrekta na vikatuzi nguvu ***'(power tillers)'*** Kilimo katika Wilaya ya Ubungo kinachangia jumla ya tani 1,007.54 za mazao ya chakula ambacho ni kiasi cha asilimia **0.65%** ya mahitaji ya chakula kwa mwaka.

SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

1. MIFUGO

Ufugaji mijni ni shughuli ya kufuga wanyama inayofanywa na watu waishio mjini wenye hadhi tofauti katika jamii kwa kutumia njia ambazo ni salama kwa binadamu na mazingira.

Ufugaji mjini katika Wilaya ya Ubungo ni wa kufungia mifugo ndani kulingana na sheria za ufugaji mjini ili kudhibiti mifugo isizurure ovyo. Watu hujishughulisha na ufugaji kwa kujipatia chakula, kipato na mbolea ambayo hutumika katika kilimo.

Kutokana na mahitaji makubwa ya nyama, mayai, maziwa na kuongeza kipato kwa jamii ufugaji mjini umekua kwa kasi kubwa. Wadau wa ufugaji mjini ni pamoja na wajasiriamali, wastaafu, wanawake, wasio na ajira rasmi, watunga sheria, wataalam wa mifugo, vibarua, Maafisa mipango, wauza vyakula na madawa ya mifugo na walaji.

Wanyama wanaofugwa katika Manispaa ya Ubungo ni ng,ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, kuku wa kienyeji, kuku wa nyama na kuku wa mayai.

MAKISIO YA WANYAMA

Aina ya mnyama /samaki	**Idadi**
Ng'ombe wa maziwa	5,027
Ng'ombe wa kienyeji	6,502
Mbuzi	2,933
Mbuzi wa maziwa	14,669
Kondoo	2,550
Nguruwe	25,360
Kuku wa nyama	1,847,411
Kuku wa mayai	240,206
Kuku wa kienyeji	1,963,043
Bata	32,381
Samaki wa maji baridi	1.8 tani
Punda	15
Mbwa	10,078

Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 idara ya Mifugo na Uvuvi ilipanga kutekeleza shughuli mbalimbali za ugani na miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na kuwezesha ukaguzi wa wanyama katika machinjio ya ng'ombe, nguruwe na kuku ili kulinda afya wanyama na binadamu.

CHANGAMOTO

- Kuathirika kwa afya ya jamii kutokana na usafi duni, vinyesi, inzi na wadudu.
- Kuahtirika kwa afya ya wanyama kutokana na uwelewa mdogo kwa wafugaji na upungufu wa huduma za ugani.
- Uchafu unaotokana na kinyesi na maji yanayotiririka toka machinjioni.
- Mitazamo hasi kwamba ufugaji mjini hauna tija.
- Ukosefu maeneo ya ufugaji kutokana na ukuaji wa mji na maeneo mengi kufanywa makazi ya watu.
- Upungufu wa wataalam wa mifugo.

MIKAKATI

Kuelimisha jamii kuhusu ufugaji mjini.

Kujenga mabanda bora ya kufugia ili kuzuia kero kama harufu, kelele na uharibifu wa mazao.

Kuimarisha utuoaji wa huduma za mifugo.

Kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira.

Kujenga machinjio ya kisasa ili kudhibiti uchinjaji holele na kilinda afya ya mlaji.

2. UVUVI - UFUGAJI WA SAMAKI

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina takribani mabwawa 30 ya kufugia samaki. Aina ya samaki wanaofugwa ni Tilapia (*Oreochromis niloticus*) na Kambale (*Clarias gariepinus*). Zaidi ya wadau 50 wanaomiliki bucha za samaki maeneo ya Shekilango, Riverside, Kimara, Mbezi, Kimara Suka, Mabibo, Sinza na Mnzese.

MAFANIKIO

- Kupungua kwa vitendo vya kuvunja sheria na taratibu za uvuvi kutokana na doria za mara kwa mara
- Kuongezeka kwa wafugaji binafsi wa samaki na kufikia zaidi ya mabwawa 30

CHANGAMOTO

- Hakuna vifaa vya kupima paramita mbalimbali za maji na kutengeneza chakula kwa ajili ya ufugaji bora na endelevu wa samaki.
- Hakuna shamba darasa, chakula bora, maji yakutosha na vituo vya kuzalisha vifaranga bora kwa ajili ya ufugaji endelevu wa samaki.
- Uhaba wa maji safi na salama kwa wafugaji wa samaki.
- Upungufu wa wataalamu wa uvuvi.

MIKAKATI

- Kujenga bwawa darasa la samaki, vituo vya kuzalisha vifaranga bora na kufanya jitihada za upatikanaji wa chakula na maji
- Kununua vifaa vya kupimia paramita mbalimbali za maji
- Kuhamasisha vyama vya wafugaji wa samaki wasajili vyama vyao kisheria ili waweze kupata ruzukukutoka wizarani na kukopesheka kwenye taasisi za kifedha
- Kuongeza wataalamu wa samaki wafike 19

SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kupitia Kitengo cha Maendeleo ya Jamii, ina majukumu ya kuratibu na kusimamia ushiriki wa Jamii katika kushiriki utekelezaji wa miradi ya Maendeleo.

CHANGAMOTO

- Mazingira ya kimji ambapo shughuli za maendeleo katika jamii kuingiliana na shughuli za binafsi hivyo kuathiri ushiriki wa jamii katika shughuli za kujitolea.
- Ukosefu wa fedha zenye kukidhi mahitaji ya Jamii maskini/za pato la chini.
- Muingiliano wa mila na desturi za kigeni
- Utegemezi miongoni mwa jamii za mjini kwa dhana kwamba Serikali itatoa kila kitu.
- Mmomonyoko wa maadili miongoni mwa jamii unaopelekea kukua kwa tatizo la watoto wanaozurura mitaani na omba omba.

SEKTA YA USTAWI WA JAMII

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kupitia Kitengo cha Ustawi wa Jamii, huratibu na kusimamia huduma za Ustawi wa Jamii, kwa kuhakikisha makundi maalumu yanapata haki za msingi wakiwemo watoto, wazee na watu wenye ulemavu. Pia kupunguza watoto wanao kinzano na sheria, kupunguza migogoro katika familia, kusimamia makao ya watoto na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na kuvisaidia kupata usajili.

Mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa shughuli za Ustawi wa Jamii.

CHANGAMOTO

i. Ongezeko la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani na wanaoishi katka mazingira hatarishi
ii. Upungufu wa Maafisa ustawi wa jamii hasa ngazi ya kata, hospitali na mahakamani. Kwa kata tunahitaji maafisa 34 ila kwa sasa wapo 7 hivyo kunaupungufu wa maafisa 27. Ngazi ya hospitali tunahitaji watumishi 10 na kwa sasa wapo 4 ivyo kuna upungufu wa watumishi 6 na ngazi ya mahakama hatuna watumishi.
iii. Ukosefu wa usafiri

iv. Ufinyu wa Ofisi
v. Ongezeko la watoto wanaokinzana na sheria.
vi. Kuwepo kwa makao ya watoto yanayoanzishwa kiholela.

SEKTA YA BIASHARA:

Idara ya Biashara ni moja ya Idara ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inayojishughulisha na kazi za utoaji wa leseni za biashara, usimamizi na uratibu wa masoko yote ya umma.

CHANGAMOTO:

- Kasi ya ongezeko la wafanyabiashara katika maeneo yasiyo rasmi
- Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kuendeleza maeneo mapya ya masoko
- Tozo dogo la ushuru lisilolingana na gharama za utoaji huduma katika masoko.
- Uvamizi wa watu binafsi waliojenga kwenye maeneo rasmi ya masoko

SEKTA YA USHIRIKA

Hadi kufikia April, 2016, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ilikuwa na idadi ya Vyama vya Ushirika 225. Kati ya hivyo SACCOS ni 115, ushirika wa Kilimo chama 1, viwanda vidogo 1, ushirika wa huduma vyama 5 na vinginevyo 3. Vyama vya SACCO's vinatoa huduma za kibenki kwa wanachama wake ambazo ni kuweka akiba na kisha kukopa, hivyo kuwawezesha kuendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi yaani biashara na maendeleo. Jumla ya vyama 19 vilivyobaki ni vyama vinavyotoa huduma mbalimbali kwa wanachama wake kwa mfano; Ushirika wa Nyumba n.k. Halmashauri inaendelea kutoa elimu kwa Vyama vya Ushirika ili viwe imara na endelevu.

CHANGAMOTO

- Idadi ya maafisa ushirika ni ndogo ukilinganisha na idadi ya vyama vya ushirika
- Ofisi ya kitengo cha ushirika ni ndogo ukilinganisha na idadi ya watumishi waliopo.
- Ucheleweshaji wa marejesho ya mikopo toka kwa wanachama wasio waaminifu.
- Wanachama kutokuweka akiba mara kwa mara katika Vyama vyao matokeo yake Vyama vingi vimekuwa na mitaji midogo na kutegemea mikopo toka Asasi za fedha
- Ucheleweshaji wa makusudi kwa watendaji kufunga vitabu vya mahesabu ya Vyama vya Ushirika.
- Baadhi ya wanachama kuogopa kukopa katika SACCOS.
- Viongozi wa SACCOS kukopeshana bila kufuata utaratibu wa SACCOS, sera kanuni na sheria
- Ukusefu fedha za kutosha kwa ajili ya mafunzo ya viongozi na wanachama wa vyama vya ushirika.
- Ukosefu wa usafiri wa kwenda na kurudi katika Vyama vya Ushirika.

MIKAKATI

- Kutoa elimu ya ushirika na ujasiriamali kwa wanachama na viongozi wa vyama vya ushirika
- Kutoa mafunzo ya utunzaji hesabu kwa watendaji wa vyama vya ushirika.
- Kushirikiana na taasisi mbalimbali za fedha kama vile mifuko ya hifadhi ya jamii, mabenki na mifuko ya serikali ili kukuza mitaji ya SACCOS.
- Kuhamasisha wananchi wengi zaidi hasahasa vijana na wanawake ili waanzishe SACCOS zao.

SEKTA YA UPIMAJI NA RAMANI, ARDHI, MIPANGOMIJI, UTHAMINI NA MALIASILI

UPIMAJI

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kupitia kitengo cha Upimaji na Ramani kimekuwa ikijihusisha na kupanga mji kwa kuboresha maeneo ya wakazi wake kwa kupima viwanja.

CHANGAMOTO

- Uhaba wa alama za msingi katika maeneo mengi ya msingi.
- Uelewa mdogo wa wananchi katika kutunza alama za Upimaji.
- Uhaba wa usafiri wa uhakika.
- Ufinyu wa Maktaba ya kutunzia Vifaa vya Upimaji, michoro ya upimaji na ramani ya Mipango mji.

MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

- Eneo la Kimara zoezi la kuandaa alama za msingi limekamilika na utaratibu wa kupima viwanja umeanza, Mikakati ya kusambaza alama za msingi Kwembe na Kibamba inaendelea.
- Utaratibu wa kutoa elimu umekuwa ukitolewa kwa viongozi wa mitaa kwa kuwa wapo karibu zaidi na wananchi.

SEKTA YA MALIASILI

UFUGAJI WA SAMAKI

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina takribani mabwawa 30 ya kufugia samaki. Aina ya samaki wanaofugwa ni Tilapia (*Oreochromis niloticus*) na Kambale (*Clarias gariepinus*). Zaidi ya wadau 50 wanaomiliki bucha za samaki maeneo ya Shekilango, Riverside, Kimara, Mbezi, Kimara Suka, Mabibo, Sinza na Mnzese.

MISITU NA HIFADHI YA MAZINGIRA

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina malengo ya kupanda **miti 692,893** ambapo wastani wa **miti 370,698** imepandwa.

UFUGAJI WA NYUKI

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina vikundi vya ufugaji nyuki **10** na wafugaji binafsi **10,** jumla ya mizinga ya kisasa **150** na mizinga ya asili **10**

MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA MALIASILI

- Kupungua kwa vitendo vya kuvunja sheria na taratibu za uvuvi kutokana na doria za mara kwa mara
- Kuongezeka kwa wafugaji binafsi wa samaki na kufikia zaidi ya mabwawa 30
- Kufanikiwa kupanda miti 370698
- Vikundi vya ufugaji nyuki kupata mafunzo juu ya ufugaji nyuki wa kisasa

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA MALIASILI

- Vituo vya kupokelea samaki havijaboreshwa mfano, havina mitambo ya kutengenezea barafu.
- Hakuna vifaa vya doria za nchi kavu (usimamizi wa sheria, kanuni, uvuvi haramu)
- Hakuna vifaa vya kupima paramita mbalimbali za maji na kutengeneza chakula kwa ajili ya ufugaji bara na endelevu wa samaki.
- Hakuna shamba darasa/ la mfano na vituo vya kuzalisha vifaranga bora kwa ajili ya ufugaji wa samaki.
- Uelewa mdogo katika kulinda na kutunza mazingira (upandaji miti na utunzaji wake)
- Bajeti ndogo ya kuhifadhi na kutunza mazingira
- Uendelezaji wa miji unapunguza maeneo ya mashamba hivyo ufugaji wa nyuki kupungua.
- Upungufu wa wataalamu wa nyuki, uvuvi na misitu.
- Ukosefu wa shamba la mfano la ufugaji nyuki na samaki.
- Uvamizi wa hifadhi ya misitu ya hifadhi.

MIKAKATI

- Kujenga bwawa darasa la samaki
- Kununua vifaa vya kupimia paramita mbalimbali za maji
- Kuhamasisha vyama vya wafugaji wa samaki wasajili vyama vyao kisheria ili waweze kupata ruzukukutoka wizarani na kukopesheka kwenye taasisi za kifedha
- Kuwa na wataalamu wa nyuki 3

KITENGO CHA MAWASILIANO NA HABARI (IT)

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo Kwa kutumia Teknolojia ya kompyuta imeweza kuhifadhi takwimu za walipa kodi Kwa kutumia mifumo ya kompyuta, kusimamia mtandao wa mawasiliano ya kompyuta, Mtandao wa ndani wa mawasiliano (LAN), kusimamia mifumo yote ya Halmashauri na Serikali Kuu inayotekelezwa katika ngazi ya Halmashauri ya Kinondoni. Mifumo iliyopo ni EPICOR (mfumo wa fedha), MRECOM (mfumo wa mapato), MOLIS(mfumo wa malipo ya ardhi), mfumo wa kuainisha walipa kodi kwa kutumia ramani (Geographical Information System), mfumo wa watumishi mishahara(LAWSON), mfumo wa Utumishi TAMISEMI (Local Government Human Resource Information System-LGHRIS), mfumo wa bajeti (Plan Rep) na mfumo wa kukusanya takwimu ngazi za kata kwa watakwimu (Local Government Monitoring Database-LGMD), na mfumo wa mahudhurio(biometric finger print attendance register system) . Vilevile Kitengo kinasimamia malipo ya kielektroniki (electronic payment system) ambayo yanafanyika chini ya wakala aliyechaguliwa na Halmashauri kwa sasa ni MAXMALIPO. Kitengo kinawezesha kutoa taarifa kwa wananchi ndani na nje ya nchi kupitia tovuti (www.ubungomc.go.tz), Mitandao ya kijamii kama vile facebook, twitter na blog (www.ubungomc.blogspot.com).

MAFANIKIO

Kwa kutumia mifumo ya Kompyuta Halmashauri imeweza:

- Kuunganisha **mifumo yetu ya malipo** na Benki ya **CRDB**
- Kuwa na **Mfumo mpya wa kieletroniki (electronic payment system)** ambapo mwananchi analipa kwa njia ya mtandao kupitia **MAXMALIPO**.
- Kutunza kumbukumbu za walipa kodi, kupanga mapato na matumizi, kusimamia malipo yote, kuweka kumbukumbu sahihi za watumishi, kupokea malipo kwa kutumia mifumo ya kompyuta yaani malipo ya ardhi na malipo ya kodi mbalimbali
- Kusimamia mahudhurio ya watumishi kwa kutumia time and attendance biometric finger print register system
- Kuwa na mtandao wa ndani ulioungwa na mkonga wa Taifa kutoka jengo hadi jengo
- Kujiunga na Mkonga wa Taifa (Optic fiber cable) ambao unarahisisha mawasiliano ya internet na mifumo mingine kama vile LAWSON, EPICOR na LGHRIS.
- Kuwepo kwa huduma ya 'Internet' kwa ajili ya mawasiliano ya ndani na nje ya nchi katika ukubwa wa 2048kbps unaotolewa na TTCL
- Kuwepo kwa program za vizuizi vya kompyuta (Antivirus) kwa ajili ya kuzuia kompyuta kushambuliwa na virusi
- Kuwepo kwa Huduma ya internet kwa kutumia (WI-FI) wireless katika kituo kipya cha Mabasi sinza.
- Kuwepo kwa huduma za internet katika ofisi za Manispaa zilizopo Mwananyamala
- Kuwepo kwa hati za madai za mradi wa viwanja vya mabwepande kwenye mfumo wa MRECOM

CHANGAMOTO

- Mabadiliko ya tekinolojia yanayohitaji mafunzo ya mara kwa mara
- Uelewa mdogo wa matumizi sahihi na salama kwa watumishi wa serikali jambo ambalo linahitaji mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi
- Mkanganyiko wa uwepo wa mifumo inayofanana na kufanya watendaji washindwe kuwa na maamuzi sahihi ya utekelezaji
- Kutokuwa na ruzuku ya serikali kwenye huduma ya intaneti na ujengaji uwezo katika tekinolojia ya mawasiliano ya kompyuta

MIKAKATI

- Kuwepo na bajeti ya mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi wa TEHAMA
- Kuweka mafunzo kwa watumishi wa Halmashauri juu ya matumizi sahihi na salama ya mifumo ya kompyuta na vifaa vyake
- Kuwepo na uwiano wa uanzishwaji mifumo ili kuondoa Mkanganyiko wa kuwa na mifumo inayofanana.
- Serikali kuu kutenga ruzuku ya mawasiliano ya intaneti na kujenga uwezo kwa watumishi wa TEHAMA.

KITENGO CHA SHERIA, ULINZI NA USALAMA

Halmashauri ya Ubungo ina kitengo cha sharia ambacho kina idadi ya wanasheria tisa (9). Kitengo hiki kina jukumu la kufanya shughughuli zote za Manispaa zinazohusiana na masuala ya kisheria. Hii ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa Mkurugenzi wa Manispaa, kutoa huduma za kisheria kwa watu mbalimbali ikishirikiana na serikali kuu, na jamii kwa ujumla. Kusimamia walinzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ili kufanikisha ufanisi wa huduma kwa wananchi na kuhakikisha sheria za nchi na sheria ndogo za Manispaa zinafatwa bila kukiukwa.

Pia kitengo cha sheria kina jukumu la kupitia mikataba yote inayoihusu Halmashauri ya Manispaa ambayo huandaliwa baada ya kupitishwa na zabuni mbalimbali za Manispaa kuhusiana na kazi za ujenzi, utoaji huduma ya uzoaji taka, huduma za Afya na mikataba ya maandalizi ya kazi mbalimbali.Takribani mikataba 400 huandaliwa kwa mwaka, pia kuandaa sheria ndogo takribani 2 mpaka 4 kwa mwaka na kutoa semina kwa mabaraza ya Kata.

Pamoja na majukumu hayo kitengo cha sheria huiwakilisha Manispaa kwenye mashauri yanaihusu katika Mahakama mbali mbali.Katika kipindi cha mwaka 2014/2015 kuna jumla kesi 350 zinazoendelea katika mahakama hizo.

CHANGAMOTO

i) Watu kutoona umuhimu wa kufuata sheria.

ii) Ongezeko la idadi kubwa ya watu katika Manispaa ya Kinondoni wanaotoka mikoani na kushukia kituo cha mabasi Ubungo, kutokana na hilo Manispaa ya Kinondoni inawawia vigumu katika utekelezaji wa sheria.

iii) Uhaba wa vitendea kazi mfano, usafiri, kompyuta, printa, vitabu vya sheria pamoja na sheria zenyewe.

iv) Ufinyu wa ofisi.

MCHANGANUO WA WADAU

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina wadau mbalimbali wanaosaidiana na Halmashauri katika kutoa huduma za jamii. Mchanganuo ufuatao unaonyesha wadau mbalimbali na matarajio yatokanayo na huduma zitolewazo na Halmashauri.

JEDWALI NA. 12: MAKUNDI YA WADAU

NA	WADAU	MATARAJIO
1.	Jamii	Huduma bora za kiuchumi na kijamii
2.	Serikali Kuu	Utawala bora na uwajibikaji
3.	Wajasiriamali wakubwa, wadogo na wa kati	Kodi za wastani, mazingira mazuri ya biashara na uwazi
4.	Wafanyakazi wa Umma	Mazingira mazuri ya kazi na marupurupu
5.	Washauri, Wakandarasi	Uwazi na utoaji zabuni wa haki
6.	Wataalam na Wasomi	Huduma bora
7.	Vijana	Kupatiwa ajira na utambuzi
8.	Wanawake	Fursa sawa kwa wote
9.	Sekretarieti ya Mkoa-RAS	Uwajibikaji na Utawala bora
10.	Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI	Huduma bora, Uwajibikaji na Utawala Bora
11.	Viongozi wa Kisiasa	Utendaji bora wenye tija kwa jamii
12.	Taasisi za Fedha	Kutoa huduma bora za kifedha na mikopo
13.	Taasisi zisizo za Kiserikali	Uwazi na Mahusiano
14.	Vyama vya Ushirika	Ushirikishwaji wa jamii
15.	Watu wenye Ulemavu	Kupata fursa sawa kama watu wasio na ulemavu
16.	Wafadhili	Uwazi na Utawala bora
17.	Wawekezaji	Uwazi, huduma bora na Utawala bora
18.	Watalii	Huduma bora, usalama na ukarimu
19.	Wakulima wadogo wadogo	Huduma bora na nzuri za ugani
20.	Asasi zisizo za Kiserikali	Mahusiano na uwazi

UCHAMBUZI WA HALI YA MANISPAA

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, inao uwezo na fursa muhimu katika kuboresha hali ya uchumi na kijamii, hivyo kupunguza umaskini katika jamii:-

Uwezo

(i) Wafanyakazi waliopata mafunzo na wenye ujuzi.

(ii) Upatikanaji wa vifaa vya ujenzi.

(iii) Mfumo mzuri wa uongozi.

(iv) Upatikanaji wa huduma za jamii kama vile shule za msingi, zahanati na vituo vya afya.

(v) Upatikanaji wa asasi za elimu ya juu/ushirika.

(vi) Upatikanaji wa asasi zisizo na Kiserikali na Vyama vya Kijamii.

(vii) Mfumo bora wa utoaji na upatikanaji wa taarifa.

Udhaifu:

(i) Upungufu wa vitendea kazi

(ii) Vyumba vya Ofisi ni vichache.

(iii) Upungufu wa watumishi katika baadhi ya idara na vitengo.

Fursa:

(i) Kuwepo kwa nguvu kazi ya uzalishaji

(ii) Ukanda mkubwa wa pwani wenye fukwe za kuvutia.

(iii) Uwezekano mkubwa wa kuwa na vyanzo vya mapato.

(iv) Kuwepo kwa maji ya kutosha ardhini.

(v) Maeneo mbalimbali ya kufanyia biashara ambayo pia ni mazuri kwa utalii.

Changamoto katika utoaji huduma:

(i) Umaskini wa jamii.

(ii) Uchache wa watumishi kwa baadhi ya idara.

(iii) Ushirikishwaji na ushiriki mdogo wa jamii katika michango ya maendeleo.

(iv) Uvunjaji wa sheria Ndogo za Halmashauri

(v) Kiwango kikubwa cha watu wanaohamia mijini kisicholingana na utoaji wa huduma.

(vi) Uhalifu ukiwemo Ujambazi wa kutumia silaha za moto, madawa ya kulevya na ukahaba.

(vii) Magonjwa ya mlipuko.

(viii) Uzalishaji mkubwa wa taka ngumu bila kuwa na nyenzo za kutosha.

(ix) Kuongezeka kwa makazi holela kunakosababishwa na kuongezeka kwa idadi ya watu

(x) Ongezeko la wafanyabiashara ndogo ndogo (Wamachinga, wapiga debe na ombaomba)

(xi) Uhaba wa maji ardhini

Vipaumbele vya bajeti ya 2016/2017

Bajeti hii imelenga katika kuboresha maisha ya wananchi na kukuza kipato cha mkazi ili kukuza uchumi wetu wa ndani. Vipaumbele vitakuwa katika maeneo yafuatayo:-

i. Kuboresha utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi kwa wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo.
ii. Kuboresha usafi wa mazingira na na ukusanyaji taka kwa kununua magari makubwa ya taka na magari madogo katika kata zote 14.
iii. Kutoa mikopo kwa wajasiliamali wa dogo kwa vikundi vya wanawake na vijana.
iv. Kuboresha miundombinu ya barabara kwa kujenga Madaraja/ Makalvati, barabara kwa kiwango cha lami, kufanya matengenezo ya kawaida ya barabara, muda maalum, maeneo korofi, njia za waenda kwa miguu ,Uboreshaji wa mto Sinza na Ujenzi wa Mifereji katika barabara za Manispaa.
v. Kulipa fidia kupisha ujenzi wa miradi mabali mbali ya maendeleo
vi. Kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa kupanua hospitali ya Sinza na ujenzi wa zahanati za kata.
vii. Kuboresha miundo mbinu ya shule za Msingi na Sekondari kwa kununua madawati, kujenga madarasa, vyoo, nyumba za walimu, maabara na ukarabati wa miundombinu.
viii. Kuboresha upatikana maji safi na salama kwa wakazi wa Ubungo kwa kujenga na kukarabati miundo mbinu ya maji.

DIRA:

Jamii iliyohamasika, inayokubalika, ikiwa na maendeleo ya kijamii na kiuchumi".

MADHUMUNI/DHAMIRA:

Kutoa huduma bora kwa jamii kupitia matumizi bora ya rasilimali, kujenga uwezo, utawala bora na utawala wa sheria na hivyo kuboresha maisha ya watu.

MALENGO NA MIKAKATI:

A) Huduma ya UKIMWI kuboreshwa na maambukizi mapya kupunguzwa

B) Uboreshaji, uendelezaji na utekelezaji kikamilifu mpango wa Taifa wa kupambana na rushwa.

C) Kuimarika kwa upatikanaji na ubora wa huduma za Jamii

D) Kuongezeka na kuboreka kwa huduma za kiuchumi na miundombinu

E) Kuimarika kwa Utawala Bora na utoaji wa huduma

F) Kuimarika kwa usimamizi wa Maliasili na Mazingira

G) Kuimarika kwa uwezo wa kiuchumi na kijinsia na Ustawi wa Jamii

H) Kuimarika kwa usimamizi wa kujikinga na maafa na milipuko ya magonjwa

SHABAHA

Ili kufikia dira, dhima na malengo ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, wadau wa maendeleo katika kila sekta wamelenga kutekeleza yafuatayo:

ELIMU – MSINGI

- Kuimarika kwa mazingira bora ya kazi kwa maafisa elimu 11 ifikapo Juni 2019
- Ujuzi na maarifa kwa maafisa 210 kuboreshwa ifikapo Juni 2019
- Kujenga mahusiano mazuri ya kielimu kati ya jamii na sekta ya elimu kutoka 35% hadi 85% ifikapo Juni 2019.
- Kuongeza idadi ya ufaulu wa wanafunzi wa darasa la IV na VII kutoka 91% hadi 98% ifikapo Juni 2019.
- Kuimarisha huduma kwa walimu 2,434 wa shule za msingi 74 ifikapo Juni 2019.
- Ujuzi na maarifa kwa walimu 120 wa Hisabati na Sayansi kuimarika ifikapo Juni 2019
- Kuongezeka kwa uandikishaji wa darasa la kwanza kutoka 13,542 hadi 14,626 ifikapo Juni 2019
- Vipaji vya wanafunzi kwa shule 74 za msingi kuongezeka ifikapo Juni 2019.
- Huduma kwa waratibu elimu 14 na walimu wa kujitolea 70 kumarishwa ifikapo Juni 2019.
- Kuboresha huduma ya kinga kwa wanafunzi 2,500 wenye mazingira duni ya shule 74 ifikapo Juni 2019.
- Kuboresha mazingira ya shule kwa ujanishaji na kutoa Elimu ya tabia ya nchi ifikapo Juni 2019.
- Huduma ya maji shuleni kwa kipindi chote cha mwaka kuboreshwa kutoka shule 18 hadi 64 ifikapo Juni 2019
- Huduma ya umeme shuleni kuongezeka kutoka shule 35 hadi kufikia shule 64 ifikapo Juni 2019

ELIMU – SEKONDARI

- Kuongeza uelewa wa Rushwa na ujuzi wa kupambana nayo kwa shule zote 27 za Sekondari hadi ifikapo Juni 2019.
- Kulipa ada kwa wanafunzi 517 yatima na wanaoishi katika mazingira magumu hadi ifikapo Juni 2019.
- Kuboresha ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha II, III,IV na VI kutoka asilimia 65% hadi 80% ifikapoJuni 2019.
- Kuboresha upatikanaji wa huduma kwa walimu 2,434 wa shule zote za sekondari ifikapo June 2019
- Kuboresha utoaji wa takwimu kwa shule 27 za sekondari ifikapo Juni 2019.
- Kuboresha mazingira yakufanyia kazi kwa shule 27 za sekondari ifikapo Juni 2019.
- Kuongeza idadi ya majengo ya sekondari kutoka 1,658 hadi 1850 ifikapo Juni 2019.
- Kuongeza idadi ya samani kutoka 31,876 hadi 46,000 ifikapoJuni 2019.

UTAWALA

- Huduma za usimamizi na uratibu katika ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa zinaimarishwa hadi kufikia 90% ifikapo 2019.
- Kuimarisha uratibu na shughuli za utawala katika ofisi ya Mstahiki Meya kufikia asilimia 90% ifikapo Juni 2019.
- Kuhakikisha watumishi 4,450 wanapatiwa huduma za msingi ifikapo Juni 2019.
- Kuwezesha huduma za mikutano kuimarika ifikapo Juni 2019.
- Ushirikishwaji na ustawi wa wananchi kuimarika ifikapo Juni 2019.

RASIRIMALI WATU

- Kuhakikisha mazingira ya kazi katika Kata na mitaa yanaboreka ifikapo Juni 2019.
- Huduma katika ofisi ya Masjala kuu inaimarika ifikapo 2019.
- Ushirikishwaji katika maamuzi unaongezeka kutoka **85% hadi 90%** ifikapo 2019.
- Uadilifu wa Watumishi **4,450** unaimarika ifikapo 2019.

- Kuhakikisha Ikama ya watumishi **4,450** inazingatiwa ifikapo 2019.
- Huduma za Usimamizi na Uratibu katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa zinaimarishwa hadi kufikia **90%** ifikapo 2019
- Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Waheshimiwa Madiwani ifikapo 2019
- Kuongeza idadi ya watumishi wenye sifa kuanzia **4,330 hadi 4,450** ifikapo 2019.

AFYA

- Kupunguza uhaba wa madawa,vifaa Tiba na visivyo Tiba kutoka 22% hadi 10% ifikapo Juni 2019.
- Kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi toka 188 hadi 178 hadi kufikia Juni 2019.
- Kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka 5 toka 11 kwa mwaka hadi 5 ifikapo Juni 2019.
- Kupunguza kiwango cha malaria kutoka asilimia 37 hadi 32 kufikia Juni 2019.
- Kuongeza utambuzi wa kifua kikuu kutoka 300 hadi 350 kufikia Juni 2019.
- Kuongeza vituo vya kutolea dawa za kifua kikuu kutoka 51 vilivyopo mpaka 54 ifikapo Juni 2019.
- Kupunguza upungufu wa wataalam wa afya kutoka asilimia 36 hadi 31 kufikia 2019.
- Kuboresha uendeshaji na usimamizi wa huduma za afya katika ngazi zote kutoka asilimia 60 hadi 80 kufikia 2019.
- Kuongeza uwezo wa kushughulika dharula na majanga kutoka asilimia 50 hadi 70 kufikia Juni 2019.
- Kuongeza uelewa wa jamii kuhusu afya na ustawi wa jamii kutoka asilimia 25 hadi 50 kufikia Juni 2019.
- Kuongeza usimamizi wa usafi wa mazingira afya na utakasaji kutoka asilimia 65 hadi 75 kufikia 2019.

- Kuongeza upatikanaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii kwa makundi yanayoishi katika mazingira hatarishi kutoka asilimia 45 hadi 60 kufikia 2019.
- Kuboresha upatikanaji wa miundo mbinu ya afya kutoka asilimia 30 hadi 50 kufikia 2019.

MAJI

- Kuongeza idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi na salama kutoka asilimia 68 hadi 81 ifikapo Juni, 2019
- Kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi 9 katika maeneo yao ya kazi ifikapo Juni, 2019

KILIMO

- Mfumo wa takwimu za kilimo (LGDM-2) kuchambuliwa na kuunganishwa katika Manispaa ya Kinondoni ifikapo Juni, 2019.
- Kuongezeka Kwa uzalishaji wa mazao ya bustani kutoka tani 10 hadi tani 12 kwa hekta ifikapo Juni, 2019.
- Wakulima wanaopata huduma za ugani kuongezeka kutoka 120,000 mpaka 135,000 ifikapo Juni, 2019.
- Kuwezesha mazingira ya utendaji kazi Kwa Watumishi 15 wa Idara ya Kilimo ifikapo Juni, 2019.
- Kuwezesha ujenzi na uwezeshaji wa kituo 1 cha kilimo katika kata ya Mabwepande ifikapo Juni, 2019.

MIFUGO NA UVUVI

- Kupuguza magojwa ya mifugo kutoka 5% hadi 2% ifikapo Juni 2019
- Kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa Watumishi 20 wa Idara ya Mifugo ifikapo Juni, 2019.
- Huduma za Ugani kuogezeka kutoka wafugaji 20,0000 hadi 25,000 ifikapo Juni 2019

- Uanzishwaji wa Benki ya takwimu za maedeleo ya mifugo na uchambuzi katika kata 10 ifikapo Juni 2019
- Kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa kutoka lita 2,000,000 hadi 3,500,000 ifikapo Jui 2019
- Uzalishaji wa mifugo wilaya ya Ubungo kuongezeka kutoka 25% hadi 75% ifikapo Juni 2019
- Utekelezaji wa sheria wa haki za wanyama katka kata 10 za Wilaya ya Ubungo (Animal Walfare Act. 2008) ifikapo Juni 2019
- Ubora wa ngozi kuongezeka kutoka 30% hadi 90% ifikapo Juni 2019
- Kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi 15 ifikapo Juni 2019
- Kuimarika kwa rasilimali za uvuvi katika kata 14 ifikapo Juni 2019
- Kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa wafanyakazi 15 ifikapo Juni 2019

UJENZI

- Kupunguza usimamizi ulio chini ya kiwango wa miradi kutoka asilimia 20 hadi 5 ifikapo Juni, 2019
- Kuongeza idadi ya barabara zinazopitika wakati wote za changarawe na lami kutoka kilomita 220.3 hadi 270.30 ifikapo Juni, 2019
- Excavator ya tairi mpya imenununuliwa na Halmashauri ambayo inatumika kusafisha na kunyoosha mito na mifereji ambayo inasaidia kupunguza mafuriko yanayosababishwa na mvua kutoka 100% mpaka 40% ifikapo Juni, 2019
- Kitengo cha matengenezo ya barabara ambacho kinasaidia kufanya kazi ndogondogo za matengenezo ya barabara ikiwemo uzibaji wa mashimo ili ziweze kupitika vizuri wakati wowote toka 30% mpaka 100% ifikapo Juni, 2019
- Kuimarisha barabara za udongo na changarawe kwa kutumia greda la manispaa kutoka kilometa 189 mpaka kilomita 427 ifikapo Juni, 2019

MIPANGO

- Tathmini na ufuatiliaji shirikishi wa miradi 200 ya maendeleo katika Kata 14 kufanyika ifikapo Juni, 2019
- Kuandaa na kupitisha bajeti ya Halmashauri miezi miwili kabla ya mwisho wa mwaka wa bajeti ifikapo Juni, 2019
- Kuongeza maeneo ya uwekezaji kutoka maeneo 10 hadi 20 ifikapo Juni, 2019
- Kuboresha mazingira ya kukusanya takwimu, kuchambua na kutunza takwimu katika Kata 14 ifikapo Juni 2019
- Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi katika idara ya Mipango na Takwimu ifikapo Juni, 2019.

FEDHA

- Kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani kutoka bilioni 46 hadi bilioni 60 ifikapo Juni, 2019.

BIASHARA

- Kuongeza masoko kutoka masoko 8 hadi 15 ifikapo Juni, 2019.
- Kukusanya na kuchambua takwimu za wafanyabiashara 5,000 ifikapo Juni, 2019.

USHIRIKA

- Kuhamasisha vikundi vya kijamii kuunda vyama vya Akiba na Mikopo ifikapo Juni, 2019
- Usimamizi wa fedha wa Vyama vya Ushirika 100 utboreshwa ifikapo Juni 2019
- Kukuza ujuzi wa uongozi na ujasiriamali kwa wanachama wa Vyama vya ushirika 100 ifikapo Juni, 2019

MAENDELEO YA JAMII

- Uhakiki wa ongezeko la ushiriki wa asasi zisizo za kiserikali (NGOs) katika kuinua maendeleo ya wanajamii kutoka 65% hadi 80% ifikapo Juni, 2019
- Kuongezeka kwa kiwango cha watu wanaopata huduma katika ofisi ya Maendeleo ya Jamii kutoka watu 5,000 hadi 10,000 ifikapo 2019
- Uwezeshaji wa vikundi 150 mbalimbali vya kiuchumi na kijamii ifikapo Juni, 2019
- Ongezeko la kiwango cha ushiriki wa jamii kaika shughuli za Maendeleo katika mitaa 197 ifikapo Juni 2019
- Upunguzaji wa kiwango cha maafa katika jamii katika kata 14 kutoka 50% hadi 80% ifikapo Juni, 2019
- Uwezeshaji wa elimu ya ujasiriamali kwa vikundi vya jamii 200 katika kata 14 kufikia Juni, 2019

USTAWI WA JAMII

- Kuboresha utoaji huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu katika kata 14 za Manispaa ifikapo Juni 2019.
- Kuboresha utoaji huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ifikapo Juni 2019.
- Kujenga uelewa wa shughuli zinazotolewa na kitengo cha ustawi wa jamii ifikapo 2019.
- Kuwezesha mazingira bora ya utendaji kazi kwa watumishi 12 wa kitengo cha ustawi wa jamii ifikapo Juni 2019.

KITENGO CHA MAWASILIANO NA HABARI (IT)

- Ukarabati wa vifaa na mifumo ya ICT kwenye Idar 13 na Vitengo 45 kufikia asilimia 80 ifikapo Juni, 2019.
- Usimamizi wa miundombinu ya ICT katika Idra 13 na Vitengo 45 kufikia asilimia 80 ifikapo Juni, 2019.

SEKTA YA MALIASILI

- Kuimarika kwa uhifadhi wa misitu katika Kata 14 ifikapo Juni, 2019
- Kuimarika kwa soko la mazao ya nyuki katika Kata 14 kufikia Juni, 2019.
- Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya nyuki katika Kata 14 kutoka lita 5,000 hadi lita 10,000 ifikapo Juni, 2019.

SHERIA ULINZI NA USALAMA.

- Kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa sheria ndogo ifikapo Juni 2019.
- Huduma za kisheria katika kata 14 itaongezeka ifikapo Juni 2019.
- Idadi ya mikataba itaongezeka kutoka 400 hadi 700 ifikapo Juni 2019.
- Idadi ya mashauri itapungua kutoka 350 mpaka 300 ifikapo Juni 2019
- Mabaraza ya Kata kuelimishwa juu ya utekelezaji wa majukumu yao yahusuyo sheria ifikapo Juni, 2019.

SERA NA MIKAKATI

Makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida na mpango wa maendeleo kwa mwaka 2016/2017 – 2018/2019 umezingatia sera na mikakati ya Kitaifa ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya millennia, Mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini (MKUKUTA), Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 – 2015, Mpango tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN), Mpango Mkakati wa 2012/2013 -2014/2015, Mipango shirikishi jamii ya fursa na vikwazo kwa maendeleo (O&OD) ya Kata na Mitaa, Sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1992 na 1997 na sera mbalimbali za kisekta. Sera hizi zimejikita katika Kuinua uchumi, Kuboresha huduma za jamii, Utawala bora na Masuala mtambuka.

UMBILE LA BAJETI

NA	KASMA	MAKUSANYO HALISI 2016-2017	BAJETI YA MWAKA 2017 - 2018	BAJETI YA MWAKA 2018 - 2019	BAJETI YA MWAKA 2019 - 2020	BAJETI YA MWAKA 2020 - 2021	BAJETI YA MWAKA 2021 - 2022
	A: MAPATO						
	A: MAKUSANYO YA NDANI						
1	MAKUSANYO YA NDANI		22,506,635,000	23,406,900,400	24,343,176,416	25,316,903,473	26,329,579,612
2	MICHANGO YA WANANCHI		750,000,000	780,000,000	811,200,000	843,648,000	877,393,920
	JUMLA YA MAKUSANYO YA NDANI	**-**	**23,256,635,000**	**24,186,900,400**	**25,154,376,416**	**26,160,551,473**	**27,206,973,532**
	B: RUZUKU YA SERIKALI KUU						
	A:MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA	**MAPOKEZI HALISI 2016-2017**	**BAJETI YA MWAKA 2017 - 2018**	**BAJETI YA MWAKA 2018 - 2019**	**BAJETI YA MWAKA 2019 - 2020**	**BAJETI YA MWAKA 2020 - 2021**	**BAJETI YA MWAKA 2021 - 2022**
1	MATUMIZI YA KAWAIDA		1,593,213,500	1,656,942,040	1,723,219,722	1,792,148,510	1,863,834,451
2	MISHAHARA		61,284,855,000	63,736,249,200	66,285,699,168	68,937,127,135	71,694,612,220
	JUMLA NDOGO	**-**	**62,878,068,500**	**65,393,191,240**	**68,008,918,890**	**70,729,275,645**	**73,558,446,671**
	B:MAPOKEZI YA RUZUKU YA MIRADI YA MAENDELEO	**MAPOKEZI HALISI 2016-2017**	**BAJETI YA MWAKA 2017 - 2018**	**BAJETI YA MWAKA 2018 - 2019**	**BAJETI YA MWAKA 2019 - 2020**	**BAJETI YA MWAKA 2020 - 2021**	**BAJETI YA MWAKA 2021 - 2022**
1	HBF		1,846,377,000	1,920,232,080	1,997,041,363	2,076,923,018	2,159,999,938
2	LGDG (CDG and CBG)		2,812,949,000	2,925,466,960	3,042,485,638	3,164,185,064	3,290,752,466
3	SEDP		718,736,000	747,485,440	777,384,858	808,480,252	840,819,462
4	Road Fund		3,573,740,000	3,716,689,600	3,865,357,184	4,019,971,471	4,180,770,330
5	NWSSP		179,962,500	187,161,000	194,647,440	202,433,338	210,530,671
6	Tanzania Strategic Cities Proect -TSCP Fund		-				
7	Other Development Grants		-				
8	ASDP/DADP		-				
9	Special Request		128,634,000	133,779,360	139,130,534	144,695,756	150,483,586
10	FREE PRI. ED. PROGRAMME		620,444,000	645,261,760	671,072,230	697,915,120	725,831,724
11	OTHER DEV GANTS		1,500,000,000	1,560,000,000	1,622,400,000	1,687,296,000	1,754,787,840
	JUMLA NDOGO		11,380,842,500	11,836,076,200	12,309,519,248	12,801,900,018	13,313,976,019
	JUMLA KUU - MAPATO:	**-**	**97,515,546,000**	**101,416,167,840**	**105,472,814,554**	**109,691,727,136**	**114,079,396,221**
	A: MATUMIZI						

NA	KASMA	MAKUSANYO HALISI 2016/17	BAJETI YA MWAKA 2017 -2018	MAOTEO YA MWAKA 2018-2019	MAOTEO YA MWAKA 2019-2020	MAOTEO YA MWAKA 2020-2021	MAOTEO YA MWAKA 2021-2022
	A: MATUMIZI YA KAWAIDA						
1	MISHAHARA FEDHA ZA NDANI		658,644,000	684,989,760	712,389,350	740,884,924	770,520,321
2	MATUMIZI YA KAWAIDA		9,093,470,000	9,457,208,800	9,835,497,152	10,228,917,038	10,638,073,720
3	MATUMIZI MIRADI YA MAENDELEO		12,754,521,000	13,264,701,840	13,795,289,914	14,347,101,510	14,920,985,571
4	MICHANGO YA WANANCHI		750,000,000	780,000,000	811,200,000	843,648,000	877,393,920
	JUMLA NDOGO	**-**	**23,256,635,000**	**24,186,900,400**	**25,154,376,416**	**26,160,551,473**	**27,206,973,532**
	B: RUZUKU YA SERIKALI KUU						
	A:MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA	**MAPOKEZI HALISI 2016/17**	**BAJETI YA MWAKA 2016 -2017**	**BAJETI YA MAPOKEZI 2017/18**	**BAJETI YA MAPOKEZI 2018/19**	**BAJETI YA MAPOKEZI 2019/20**	**BAJETI YA MAPOKEZI 2020/21**
1	MISHAHARA		61,284,855,000	63,736,249,200	66,285,699,168	68,937,127,135	71,694,612,220
2	MATUMIZI YA KAWAIDA		1,593,213,500	1,656,942,040	1,723,219,722	1,792,148,510	1,863,834,451
	JUMLA NDOGO	**-**	**62,878,068,500**	**65,393,191,240**	**68,008,918,890**	**70,729,275,645**	**73,558,446,671**
	B:MAPOKEZI YAFEDHA ZA MIRADI MIRADI	**MAPOKEZI HALISI 2016/17**	**BAJETI YA MWAKA 2016 -2017**	**BAJETI YA MAPOKEZI 2017/18**	**BAJETI YA MAPOKEZI 2018/19**	**BAJETI YA MAPOKEZI 2019/20**	**BAJETI YA MAPOKEZI 2020/21**
1	HBF		1,846,377,000	1,920,232,080	1,997,041,363	2,076,923,018	2,159,999,938
2	LGDG (CDG and CBG)		2,812,949,000	2,925,466,960	3,042,485,638	3,164,185,064	3,290,752,466
3	SEDP		718,736,000	747,485,440	777,384,858	808,480,252	840,819,462
4	Road Fund		3,573,740,000	3,716,689,600	3,865,357,184	4,019,971,471	4,180,770,330
5	NWSSP		179,962,500	187,161,000	194,647,440	202,433,338	210,530,671
6	Tanzania Strategic Cities Proect -TSCP Fund		-	-	-	-	-
7	Other Development Grants		-	-	-	-	-
8	ASDP/DADP		-	-	-	-	-
9	Special Request		128,634,000	133,779,360	139,130,534	144,695,756	150,483,586
10	FREE PRI. ED. PROGRAMME		620,444,000	645,261,760	671,072,230	697,915,120	725,831,724
			1,500,000,000	1,560,000,000	1,622,400,000	1,687,296,000	1,754,787,840
	JUMLA NDOGO		**11,380,842,500**	**11,836,076,200**	**12,309,519,248**	**12,801,900,018**	**13,313,976,019**
	JUMLA KUU YA HALMASHAURI		**97,515,546,000**	**101,416,167,840**	**105,472,814,554**	**109,691,727,136**	**114,079,396,221**